# Waliogonganisha vyeti

NA MWANDISHI WETU

MADUDU ya watumishi wenye vyeti feki yamezidi kujitokeza baada ya Tanzania Daima kunasa orodha yao ikionesha jina moja likitumiwa na watu zaidi ya watatu waliotumia cheti kimoja kupata ajira.

Katika orodha hiyo lipo jina moja linalotumiwa na watu wawili kwenye eneo moja huku watu watatu wakitumia jina moja wakiwa katika maeneo tofauti wakitofautiana namba za kuajiriwa.

Mgongano wa majina kwenye cheti kimoja, umesababisha Serikali kushindwa kujua mtumishi yupi mwenye cheti halali, hivyo wametakiwa kwenda kuthibitisha.

Hivi karibuni Serikali ilifanya uhakiki kwa wafanyakazi 435,000 ambapo kati yao watumishi 9,932 walibainika kuwa na vyeti vya kugushi huku wafanyakazi 1,538 vyeti vyao vina utata kutokana na kutumiwa na watu zaidi ya mmoja na 11,596 waliwasilisha vyeti vya kitaaluma bila vyeti vya elimu.

Orodha hiyo inaonesha kuwa watumishi walionaswa kutumia cheti kimoja wanatoka katika halmashauri za wilaya nchini, wakituhumu katika taasisi na idara mbalimbali za Serikali.

Katika orodha hiyo, wamo ... halmashauri ya wilaya ya Hanang na namba yake ya ajira ni 3810.

Kwa mujibu wa orodha hiyo, mtumishi Ester Paul mwenye namba ya ajira 1797, ameajiriwa katika halmashauri ya wilaya ya Bukombe wakati Ester Paul mwingine ameajiriwa katika halmashauri ya Jiji la Mbeya akitumia namba ya ajira 4590.

Orodha hiyo ambayo itawekwa hapo chini, inaonesha kuwa watumishi watatu wenye majina yanyofanana wamepata ajira katika halmashauri tatu tofauti kwa kutumia cheti kimoja.

Watumishi hao ni Fatuma Mussa ambaye amejiriwa katika halmashauri ya wilaya ya Kongwa kwa namba 683, Fatuma Mussa mwingine mwenye namnba ya ajira 3247, ameajiriwa katika halmashauri ya wilaya ya Mwanga na Fatuma Mussa wa tatu ameajiriwa katika halmashauri ya wilaya ya Handeni (V) kwa namba ya ajira 8038.

Habari ambazo Tanzania Daima imezipata, zinasema kuwa majina hayo yaliyogongana kwenye vyeti, huenda yakatangazwa Mei 10 mwaka huu wakati Serikali itakapowasilisha awamu ya pili ya uhakiki wa vyeti feki kwa watumishi wa wizara nyingine ...

| | | |
|---|---|---|
| 3511 | KILWA | HADIJA SAID |
| 7253 | BARIADI (M) | HADIJA SAID |
| 8313 | LUSHOTO | HALIMA RASHID KANIKI |
| 8314 | LUSHOTO | HALIMA RASHID KANIKI |
| 1503 | CHAMWINO | HAPPY GERSON |
| 3335 | ROMBO | HAPPY GERSON |
| 6169 | KIBAHA (M) | HERRIETH MLANGWA |
| 8481 | MUHEZA | HERRIETH MLANGWA |
| 8322 | LUSHOTO | IDRISSA MDOE ABEID |
| 8323 | LUSHOTO | IDRISSA MDOE ABEID |
| 6734 | NAMTUMBO | INNOCIATA A MUHORO. |
| 6948 | TUNDURU | INNOCIATA A MUHORO |
| 1147 | TEMEKE | JAMILA ISSA |
| 5253 | MASASI (V) | JAMILA ISSA |
| 4948 | MOROGORO (V) | JOHN MASANJA |
| 7099 | MSALALA | JOHN MASANJA |
| 2654 | MPANDA (V) | JOSEPHINE FRANCIS |
| 2686 | MPANDA MANISPAA | JOSEPHINE FRANCIS |
| 5863 | UKEREWE | LAMECK N. IGOKO |
| 5864 | UKEREWE | LAMECK N. IGOKO |
| 3780 | BABATI (V) | MAGRETH EDWARD |
| 5318 | NANYUMBU | MAGRETH EDWARD |
| 5355 | RAS MTWARA | MAGRETH JOSEPH |
| 8056 | HANDENI (V) | MAGRETH JOSEPH |
| 2349 | BUKOBA (V) | MAGRETH NGAIZA |
| 2500 | MISENYI | MAGRETH NGAIZA |
| 1816 | BUKOMBE | MARIAM JUMA |
| 3195 | MOSHI MANISPAA | MARIAM JUMA |
| 966 | KINONDONI | MARIAM RASHID |
| 8662 | TANGA JIJI | MARIAM RASHID |
| 5257 | MASASI (V) | MARIAMU HAMISI |
| 5394 | TANDAHIMBA | MARIAMU HAMISI |
| 8351 | LUSHOTO | MARY ABEL MNTAMBO |
| 8352 | LUSHOTO | MARY ABEL MNTAMBO |